

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA TATU**

**KIKAO CHA ISHIRINI**

**30 APRILI, 2021**



# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA ISHIRINI – TAREHE 30 APRILI, 2021

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

163. **MHESHIMIWA EMMANUEL ADAMSON  
MWAKASAKA (TABORA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali imechukua hatua gani kukabiliana na upungufu wa Walimu na madawati hasa baada ya Elimu ya Msingi na Sekondari kuwa bure.

164. **MHESHIMIWA NASHON WILLIAM  
BIDYANGUZE (KIGOMA KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Watumishi waliohamishiwa Halmashauri ya Uvinza kutoka Halmashauri ya Kigoma Vijijini watalipwa stahiki zao.


**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**165. MHESHIMIWA NUSRAT SHAABAN HANJE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, ni kwanini Serikali haioni umuhimu wa kurekebisha mfumo wa elimu na kuingiza

- mbinu tete na stadi za maisha ili kuwajengea uwezo wa kiushindani Vijana wanaohitimu na kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira.



**WIZARA YA MAJI:**

**166. MHESHIMIWA MINZA SIMON MJIKA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-


Je, ni lini mradi wa maji wa Ziwa Victoria utapelekwa katika Mkoa wa Simiyu hususan katika Wilaya ya Meatu kama inavyoelezwa katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

**167. MHESHIMIWA SILVESTRY FRANCIS  
KOKA (KIBAHA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itaanza na kumaliza Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Makofia – Mlandizi – Vikumburu kupitia Mbwawa kwa kiwango cha lami ambayo ipo kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi.



**DODOMA  
30 APRILI, 2021**

**S. KAGAIGAI  
KATIBU WA BUNGE**